



Jarida la Mtandaoni

TOLEO LA SEPTEMBA 2020

NSSF YAJA NA MKAKATI KULETA MABADILIKO KATIKA HUDUMA

Na MWANDISHI WETU

"Ukifanya kazi kwa mazoea haiwezekani
yakawepo mabadiliko"

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi wa Rasilimali watu na Utawala wa NSSF, Julius Mganga wakati wa mafunzo yenye lengo la kuongeza ufanisi katika utendaji kazi yanayofanyika ofisi zote za NSSF.



Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) limeendelea na mkakati wa kubadilisha mitazamo ya wafanyakazi wake ili kuleta mabadiliko katika utendaji kazi na hivyo kuleta tija.

Bw. Mganga anasema kuwa mfanyakazi yejote anatakiwa ajue wajibu wake ili kutoa huduma bora.

Hivyo NSSF imeendelea na mafunzo maalumu kwa wafanyakazi wake yanayolenga kuchochea mabadiliko katika utendaji kazi.

Bw Mganga anasema kuwa mafunzo hayo yanawafanya wafanyakazi kuondokana na utendaji kazi wa mazoea.

"Tunataka wafanyakazi wetu wabadi like na kujiona kuwa wao ni watumishi wa umma na hivyo wana wajibu wa kutoa huduma bora."

Inatoka ukurasa wa 1

Mafunzo hayo, yenye lengo la kuongeza ufanisi katika utendaji kazi yanafanyika katika ofisi zote za NSSF.

Katika mwezi wa Septemba 2020, mafunzo hayo yamefanyika katika mikoa ya Pwani, Morogoro, na Dodoma.

Bw Mganga amesema kuwa mafunzo hayo yanawaelimisha wafanyakazi kuhusu utendaji bora wa kazi katika kuhudumia wanachama.

Katika mafunzo hayo Bw. Mganga alitumia mfano wa mwili wa binadamu kuwa kielelezo cha utendaji kazi wenye ufanisi kwa kufanya kazi kwa pamoja.

"Shirika lina idara tofauti tofauti na zinafanya kazi kwa kutegemeana kama viungo vyta mwili wa binadamu" amesema Bw. Julius Mganga.

NSSF ina majukumu manne kisheria ambayo ni kuandikisha wanachama, kukusanya michango, kuwekeza na kulipa mafao kwa wanachama.

"Tumedhamiria kuboresha huduma zetu na wanachama waone kweli wanapata huduma bora," amesema Mkurugenzi huyo.

Mafunzo yachochea huduma bora kwa wafanyakazi wa NSSF



Wafanyakazi wa Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) wameonesha utayari wao wa kutoa huduma bora zaidi kwa wanachama wa Shirika hilo.

Baadhi ya wafanyakazi wa Shirika hilo kutoka katika mikoa ya Morogoro na Dodoma wametoa kauli hizo mara tu baada ya kupata mafunzo ya jinsi yakukabiliana na mabadiliko yenye lengo la kutoa huduma bora kwa wanachama, wadau na Jamii kwa ujumla.

JARIDA LA MTANDAONI LA NSSF

TOLEO LA SEPTEMBA 2020



**Hizi ni hisia za wafanyakazi mara baada ya kupata
mafunzo hayo**

“Mafunzo yameniongezea ujuzi zaidi katika kutoa huduma bora kwa wanachama.”

Elizabeth Maduga, Mtunza Kumbukumbu Msaidizi wa NSSF Morogoro



JARIDA LA MTANDAONI LA NSSF

TOLEO LA SEPTEMBA 2020



"Mimi katika nafasi yangu ya utawala nitajitahidi kuwa mstari wa mbele katika kuhamasisha na kuweka mafunzo hayo katika vitendo,"

John Joel, Afisa Utawala NSSF Dodoma.



"Tumejipanga kutoa elimu kwa waajiri ili walete michango kwa wakati na tuweze kutoa huduma kwa wakati."

Filomena Shirima, Afisa Huduma kwa wateja NSSF Dodoma.



"Sasa tupo kwenye mabadiliko ya kiutendaji, tunahitaji utayari wa wanachama kupokea huduma bora."

Hussein Doto, Afisa Matekelezo NSSF Dodoma

Na MWANDISHI WETU

Katika kuhakikisha kuwa wanachama wanapata huduma bora, Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) lina madawati ya malalamiko katika ofisi zake zote.

Kupitia madawati hayo, Shirika linapokea kero na malalamiko kutoka kwa wanachama na kuyafanyia kazi kwa ajili ya kuboresha huduma.

Mkurugenzi wa Rasilimali watu na Utawala wa NSSF, Bw. Julius Mganga amewahimiza wanachama wa Shirika hilo kutumia madawati ya malalamiko yaliyopo katika kila ofisi ya shirika hilo kupeleka kero zao ili huduma ziboreshwé zaidi.

Ametoa kauli hiyo jijini Dodoma alipokuwa anatoa mafunzo yanayolenga mabadiliko ya kiutendaji kwa wafanyakazi wa NSSF.

Mafunzo hayo, yenye lengo la kuleta mabadiliko na kuwandaa wafanyakazi namna ya kukubali mabadiliko, yanafanyika

NSSF: TUMIENI MADAWATI YA MALALAMIKO KUTATUA KERO

katika ofisi za NSSF za Lakini pia anaweza Mikoa na tayari kuwasilisha malalamiko kwa njia ya barua pepe; **customercare@nssf.or.tz** au anaweza kupiga simu ya bure kwa namba; **0800116773**

Kwa mwanachama ambaye hataridhika na utatuzi wa kero yake katika madawati yaliyowekwa ana nafasi ya kuwasilisha malalamiko yake moja kwa moja kwa meneja wa NSSF katika Mkoa husika.



"Tumewe ka madawati ya malalamiko kusikiliza kero katika ofisi zetu zote, madhumuni yetu ni yale yale kuhakikisha kuwa wanachama wetu wanapata huduma bora,"

Julius Mganga Mkurugenzi wa Rasilimali watu na Utawala NSSF

JARIDA LA MTANDAONI LA NSSF

TOLEO LA SEPTEMBA 2020



Tunajenga Maisha yako
ya Sasa na Baadae

KARIBU TUKHUDUMIE

Mitando ya kijamii ya NSSF

Facebook @ Nssf Tanzania

Twitter @NssfTanzania

Instagram @NssfTanzania

Youtube @NssfTanzania

Kituo cha miito ya simu

Simu Bure 0800116773

Huduma kwa wanachama

customercare@nssf.or.tz

Tovuti

www.nssf.or.tz

Tunajenga Maisha Yako
ya Sasa na Baadae

NSSF